# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU MATOKEO YA UTAFITI WA MAPATO NA MATUMIZI YA KAYA BINAFSI (HBS) TANZANIA BARA 2011/12, TAREHE 14 NOVEMBA, 2013

**Ndugu Wanahabari,** Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Wizara ya Fedha iliendesha Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi Tanzania Bara katika mwaka 2011/12. Utafiti huu ulikusanya, kuandaa na kuchambua taarifa za mapato, matumizi na manunuzi ya kaya. Kutokana na taarifa hizi ni rahisi kutathmini Sera mbalimbali za kijamii na uchumi pamoja na kutambua makundi ya watu yaliyoko kwenye mazingira hatarishi. Kama tafiti nyingine zilizopita, Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa mwaka 2011/12 umelenga kutoa viashiria vitakavyosaidia kufuatilia na kutathmini maendeleo ya sekta mbalimbali zilizoainishwa kwenye Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUKUTA II) Tanzania. Takwimu zilizokusanywa zilihusu watu na kaya katika maeneo yafuatayo:

- Elimu na afya ya Wanakaya;
- Manunuzi na matumizi ya kaya;
- Umiliki wa vifaa na rasilimali;
- Makazi na vifaa vya ujenzi;
- Upatikanaji wa huduma na vifaa;
- Upatikanaji wa maji na usafi wa mazingira;
- Shughuli za kiuchumi na ajira;

- Utalii;
- Umiliki wa biashara zisizo za kilimo; na
- Shughuli za kilimo.

**Ndugu Wanahabari,** Utafiti huu ulifanyika kuanzia mwezi Oktoba 2011 hadi Oktoba 2012 ambapo jumla ya kaya 10,186 kati ya 10,400 zilizokuwa zimelengwa zilihojiwa kutoka katika maeneo ya Dar es Salaam, maeneo mengine ya mjini na vijijini, Tanzania Bara. Kila kaya iliyochaguliwa ilihojiwa juu ya masuala yote yaliyotajwa hapo juu pamoja na kujaza kijitabu cha kumbukumbu ambacho kaya ilitakiwa kuandika mapato na matumizi ya kila siku kwa muda wa siku 28 mfululizo. Kijitabu hiki cha kumbukumbu kililenga katika kupata matumizi ya moja kwa moja (hasa chakula) ya kaya pamoja na matumizi mengine yasiyo ya chakula kwa kipindi hicho cha siku 28.

**Ndugu Wanahabari,** Kabla sijatoa matokeo halisi ya hali ya umaskini nchini kwa kipindi cha mwaka 2011/12 nieleze tafsiri iliyotumika kwanza; umaskini wa chakula ulitumia kigezo cha kipato cha chini ya shilingi 26,085 kwa mtu mzima kwa mwezi na umaskini wa mahitaji ya msingi ni kipato cha chini ya shilingi 36,482 kwa mwezi.

**Ndugu Wanahabari,** Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa kiwango cha umaskini wa chakula na ule wa mahitaji ya msingi ni tatizo zaidi kwa Wananchi wa vijijini ikilinganishwa na Wananchi wanaoishi mjini hususan Dar es Salaam na maeneo

mengine ya mjini. Wakati wastani wa kitaifa wa kiwango cha umaskini wa chakula ni asilimia 9.7, kiwango hicho kinafikia asilimia 11.3 kwa maeneo ya vijijini. Dar es Salaam ina kiwango cha chini kabisa cha umaskini wa chakula cha asilimia 1.0 ambapo Wananchi wanaoishi maeneo mengine ya mjini wana umaskini wa chakula wa asilimia 8.7.

Kwa upande wa umaskini wa mahitaji ya msingi, wastani wa Tanzania Bara ni asilimia 28.2 ukilinganishwa na asilimia 33.3 kwa maeneo ya vijijini na asilimia 21.7 kwa maeneo mengine ya mjini. Dar es Salaam ina kiwango cha chini cha umaskini wa mahitaji ya msingi cha asilimia 4.1.

**Ndugu Wanahabari,** Matokeo haya ya viwango vya umaskini ni kwa mujibu wa vigezo vya umaskini kwa mwaka 2011/12. Ulinganishaji wa mwelekeo wa umaskini na tafiti za Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi zilizopita utaainishwa kwenye Ripoti Kuu ikizingatiwa kuwa maboresho mengi ya mbinu za utafiti yamefanyika katika utafiti wa mwaka 2011/12 hivyo ulinganishi na uchambuzi wa taarifa unahitaji umakini na unafanyiwa kazi.

**Ndugu Wanahabari,** Utafiti huu pamoja na kutathmini kiwango cha umaskini kwa kutumia kipato, umeangalia masuala mengine ambayo siyo ya umaskini wa kipato moja kwa moja. Baadhi ya masuala hayo ni pamoja na ukuaji wa elimu ya sekondari, matumizi ya nishati ya umeme, hali ya makazi, umiliki wa baadhi ya rasilimali na mengineyo.

**Ndugu Wanahabari**, Matokeo ya utafiti huu yanaonesha jitihada za Serikali katika kuongeza ujenzi wa shule zaidi hasa zile za sekondari ambazo zimewezesha kupanda kwa kiwango cha wanafunzi wanaojiunga katika elimu ya sekondari kwa karibu mara mbili, kutoka asilimia 15 mwaka 2007 hadi asilimia 29 mwaka 2011/12.

Matumizi ya nishati ya umeme katika maisha ya kila siku ya Wananchi katika kaya ni eneo lingine ambalo Serikali imelenga kuliboresha katika jitahada zake za kuboresha maisha ya Wananchi. Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kuwa kaya zinazotumia umeme angalau kwa ajili ya mwangaza wa ndani zimeongezeka kutoka asilimia 13 kwa mwaka 2007 hadi asilimia 18 kwa mwaka 2011/12.

**Ndugu Wanahabari,** Kumekuwepo pia na ongezeko la kaya zinazoishi katika nyumba zilizojengwa kwa vifaa vya ujenzi vya kisasa tangu mwaka 2007. Utafiti unaonesha kuwa asilimia 46 ya kaya zinaishi katika nyumba zilizojengwa kwa kuta imara ikilinganishwa na asilimia 33 ya kaya zilizokuwa zinaishi katika nyumba zilizojengwa kwa kuta imara mwaka 2007. Kwa upande mwingine, asilimia 66 ya kaya zinaishi katika nyumba zilizoezekwa kwa paa la kisasa (bati, asbestos, vigae, zege, n.k.) ikilinganishwa na asilimia 55 ya kaya zilizokuwa zikiishi katika nyumba zenye paa la kisasa mwaka 2007.

**Ndugu Wanahabari,** Utafiti pia unaonesha kuwa asilimia 4 ya kaya zinamiliki pikipiki, asilimia 55 zinamiliki redio, na asilimia 57 ya kaya zote zina angalau mwanakaya mmoja anayemiliki simu ya mkononi. Umiliki wa simu za mkononi unatofautiana sana kwa maeneo. Wakati kiasi cha asilimia 78 ya kaya za maeneo mengine ya mjini na asilimia 88 ya kaya za Dar es Salaam zinamiliki angalau simu moja ya mkononi, asilimia 45 ya kaya za vijijini zinamiliki angalau simu moja ya mkononi.

**Ndugu Wanahabari,** Utafiti huu uligusa masuala mengi yaliyo ya msingi kwa Wapanga Mipango, Watunga Sera, Wafanya Maamuzi, Serikali na umma kwa ujumla ambayo bado yanafanyiwa uchambuzi na matokeo yake yatawasilishwa katika chapisho litakalotoka kabla ya mwisho wa mwaka huu. Masuala kama kiwango cha elimu kwa watu wazima, upatikanaji wa maji safi na salama, upatikanaji wa huduma za afya, shughuli za kiuchumi, biashara za kaya, na utalii ni baadhi ya masuala yatakayokuwemo katika chapisho hilo.

**Ndugu Wanahabari,** Ombi langu kwenu nyote ni kuhakikisha kwamba matokeo haya ambayo ni ya muhimu sana kwa ajili ya kuboresha hali ya maisha ya Wananchi, na mengineyo yatakayotokana na utafiti huu, yamfikie kila mmoja kupitia kwenu kwani kila mmoja wetu ni mdau wa utafiti huu. Takwimu hizi ni za msingi kwa Serikali na kwa wadau wengine wa sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii katika kuhakikisha

upatikanaji wa huduma zinazokidhi viwango vya ubora kwa ajili ya watu wote wa nchi hii.

**Ndugu Wanahabari,** Nichukue fursa hii kutoa shukrani za dhati za Serikali na kwa wanachi katika kaya zilizochaguliwa kwa kutenga muda wao ili kufanikisha malengo ya utafiti huu kwa kushirikiana na watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Pia kwa msaada wa kiufundi uliotolewa na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa (DFID) ya Uingereza bila kuwasahau wadau wengine wa maendeleo ambao wamekuwa na mchango mkubwa siyo tu katika utafiti huu bali katika jitihada mbali mbali za Serikali katika kutoa huduma kwa wanachi wake.

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**